



Tingi na ng'ombe

 Ingrid Schechter

 Ingrid Schechter

 Matteo E. Mwita

 2

 Kiswahili SW



Tingi aliishi na bibi yake.



Alizoea kuchunga ng'ombe na bibi yake.



Siku moja wanajeshi walikuja.



Wakawachukua ng'ombe.



Tingi na bibi yake walikimbia na kujificha.



Walijificha kichakani hadi usiku.



Wanajeshi walirudi tena.



Bibi alimficha Tingi chini ya majani.



Mwanajeshi mmoja alimkanyaga, lakini akanyamaza kimya.



Wanajeshi walipoondoka Tingi na bibi yake wakajitokeza.



Wakajikongoja kimya kimya kurudi nyumbani.



Global Storybooks

globalstorybooks.net

Tingi na ng'ombe

 Ingrid Schechter

 Ingrid Schechter

 Matteo E. Mwita

